# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.7 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) SEPTEMBA 2021

# MWELI ATAKA MIKOA, HALMASHAURI KUWA NA KANZIDATA ZA WADAU WANAOTOA HUDUMA YA ELIMUMSINGI



*Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Gerald Mweli akitoa hotuba ya kufunga kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi. Kikao kazi hicho kilichoandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kilifanyika Agosti 16-18, 2021 jijini Dodoma.*

## NUKUU



"…….inasikitisha sana pale ambapo unakuta mwalimu anaajiriwa lakini baada ya muda anafukuzwa kazi na wakati huo kuna watu nyuma yake ambao kuishi kwao kunategemea ajira yake"

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# SHIME TUKACHANJE, CHANJO SASA RUKSA KWA WOTE

Serikali imetangaza fursa kwa wote wanaotaka kupata huduma ya chanjo dhidi ya virusi vya Corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu (UVIKO-19).

Hatua hii imekuja baada ya kuwapo mwamko mkubwa wa Watanzania wakiongozwa na viongozi wa Serikali, Siasa, Dini, Jumuiya, na makundi mbalimbali kutaka chanjo hiyo tangu huduma hiyo ilipozinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Itakumbukwa kuwa hapo awali chanjo hii haikuwa inatosheleza kila Mtanzania aliyekuwa anahitaji kuchanjwa hivyo, Serikali iliweka makundi ya kipaumbele katika kupata huduma hiyo wakiwamo watumishi wa sekta ya afya, wazee na watu wenye magonjwa sugu au yale ya kudumu.

Serikali yetu iliendelea kufanya jitihada za kuagiza chanjo zaidi ambapo hadi sasa chanjo ya UVIKO-19 ipo ya kutosha na kila mtu kwa hiari yake anaweza kuipata bila kujali makundi kama ilivyokuwa hapo awali.

Ni wazi kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amefanya jitihada kubwa katika kujali na kulinda afya za Watanzania. Hivyo basi, tunawahimiza Walimu na Watanzania wote kwa ujumla ambao bado hawajapata chanjo hii kuendelea kujitokeza katika vituo vilivyo karibu yao ili wakachanjwe.

Tumeshuhudia viongozi wetu mbalimbali wakijitokeza kupata chanjo, hivyo ni vyema kila mmoja wetu akaona umuhimu wa jambo hili katika kulinda afya yake na kulinda wengine.

Pamoja na hayo, tunaendelea kusisitizwa kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 kama vile kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kukaa umbali usiopungua mita moja kutoka mtu mmoja mpaka mwingine, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara, kutumia barakoa na kutumia vitakasa mikono pale hali inaporuhusu.

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama


**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# KATIBU TSC ASIKITISHWA NA WALIMU WANAOHITIMISHA UTUMISHI KWA KUFUKUZWA KAZI




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akijibu hoja mbalimbali za walimu waliohudhuria kongamano la walimu wenye ulemavu kutoka Wilaya za Tanzania Bara lililofanyika Agosti 20-21, 2021 jijini Dodoma. Kongamano hilo liliandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).*



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo akiwasilisha mada kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishi wa Walimu katika kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililofanyika Agosti 20-21, 2021 jijini Dodoma. Kongamano hilo liliandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).*

**Na Mwandishi Wetu.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amesema anaumizwa na walimu kuhitimisha utumishi wao kwa kufukuzwa kazi kutokana na kuwa na tabia zinazokwenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Nkwama ameyasema hayo wakati akijibu maswali yaliyoulizwa na walimu kuhusu taratibu mbalimbali za utumishi wa walimu katika kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape akiwasilisha mada kuhusu Historia ya TSC pamoja na Nguzo za Maadili ya Kazi ya Ualimu katika kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililofanyika Agosti 20-21, 2021 jijini Dodoma. Kongamano hilo liliandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).*

# KATIBU TSC ASIKITISHWA NA WALIMU WANAOHITIMISHA UTUMISHI KWA KUFUKUZWA KAZI

Katika kongamano hilo lililofanyika Agosti 20-21, 2021 jijini Dodoma, Nkwama alieleza kuwa Serikali inapomwajiri mwalimu inatarajia mtumishi huyo adumu katika utumishi wake hadi pale atakapotimiza umri kustaafu kwa mujibu wa sheria au kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa mwanadamu.

"Mara nyingi mwalimu anaajiriwa akiwa kijana na sisi tunatarajia kuwa atadumu katika utumishi wa umma na kufaidi haki zake zote hadi umri wake wa kustaafu utakapofika. Lakini kwa kweli inasikitisha sana pale ambapo unakuta mwalimu anaajiriwa lakini baada ya muda anafukuzwa kazi na wakati huo kuna watu nyuma yake ambao kuishi kwao kunategemea ajira yake," alisema Nkwama.

Alifafanua kuwa TSC imejikita katika kuwaelimisha walimu juu ya taratibu za utumishi wao ili watekeleze majukumu yao bila kuvunja taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2016.

Aliendelea kueleza kuwa pamoja na kupungua kwa mashauri ya nidhamu kutokana na jitihada za kutoa elimu, bado kuna walimu wachache ambao wanaojihusisha na vitendo vinavyokwenda kinyume na Miiko na Maadili ya kazi ya ualimu na kujikuta wakikatisha ajira zao kwa kufukuzwa kazi.

"Tumefanya jitihada mbalimbali za kutumia kila fursa inayopatikana kwa ajili ya kuwaelimisha walimu, tunashukuru kuona kwamba kuna mabadiliko. Lakini sisi lengo letu ni kuona kila mwalimu anazingatia yale aliyoelekezwa, tunaumia tukiona bado kuna walimu wanaofukuzwa kazi," alisema Katibu wa TSC.




*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka TSC, Moses Chitama akiwasilisha mada kuhusu Muundo wa Tume hiyo katika kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililofanyika Agosti 20-21, 2021 jijini Dodoma. Kongamano hilo liliandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).*

Katibu huyo alisisitiza kuwa pale TSC inapoendesha shauri la nidhamu la mtu inahakikisha inasimama katika haki kwa mujibu wa sheria bila kupendelea au kumuonea mtu, na pale inapotokea kuna upande usioridhika na uamuzi kuna haki ya kukata rufaa kwa mujibu wa sheria.

"Hapa tunashauriana na kuelimishana ili tuzingatie sheria kwenye utendaji wetu wa kazi lakini linapokuja shauri la nidhamu, hapo hakuna muda wa mjadala tena tunachoangalia ni sheria peke yake, kama mwalimu atakutwa na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria na kama hajapatikana na hatia ataachiwa huru," alieleza Nkwama.

Akiongelea suala la haki kwa mtuhumiwa wa shauri la nidhamu, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoa TSC, Wakili Richard Odongo alieleza kuwa mtuhumiwa ana haki ya kupewa hati ya mashtaka inayoeleza kosa, wakati na namna kosa lilivyofanyika.

Aliongeza kuwa mtuhumiwa lazima apewe muda wa kutosha kujitetea na endapo hatawasilisha

# KATIBU TSC ASIKITISHWA NA WALIMU WANAOHITIMISHA UTUMISHI KWA KUFUKUZWA KAZI



*Walimu wenye mahitaji maalum wakifuatilia mada kuhusu masuala ya TSC kupitia mkalimani wa lugha ya alama.*



*Mwalimu Hellen Mbando kutoka Kilimajaro akiuliza swali mara baada ya viongozi kutoka TSC kuwasilisha mada wakati wa kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililofanyika Agosti 20-21, 2021 jijini Dodoma.*

utetezi, utetezi aliowasilisha haujitoshelezi au amekanusha tuhuma ni lazima iundwe kamati ya uchunguzi kwa ajili ya kuchunguza shauri hilo.

Odongo alieleza sifa za wajumbe wa kamati ya uchunguzi kuwa lazima wawe watumishi wa umma, wawe wamefikia cheo cha uandamizi au zaidi, wawe na cheo kikubwa zaidi ya anayechunguzwa na kamati hiyo inatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua wawili na wasiozidi wanne huku ikisisitizwa kuzingatia jinsi.

Wakili huyo alihitimisha mada yake kwa kueleza haki za mwalimu anayechunguzwa kuwa ni kujulishwa muda, siku, mahali na tarehe ambapo uchunguzi wa shauri lake utafanyika, kuwepo au kuwa na uwakilishi wakati wa uchunguzi wa shauri lake, kuhoji mashahidi na kupewa kielelezo chochote kinachotumiwa kama ushahidi dhidi yake.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape, alieleza kuwa tangu Tanzania ipate uhuru walimu wamekuwa na chombo cha kushughulikia utumishi wao ikiwa ni juhudi za serikali kutambua umuhimu wa kundi hilo.

Alieleza kuwa walimu wana kazi kubwa kwani wao ndio wenye jukumu la kutengeneza watu wenye uwezo wa kufikia malengo ya Taifa kwa kuwa wanaanza kumjenga mwanafunzi tangu akiwa mtoto hadi anapokuwa mtu mzima, amesisitiza walimu kuwa wazalendo na kufanya kazi kwa weledi ili Tanzania iendelee kupiga hatua zaidi katika maendeleo.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka TSC, Moses Chitama aliwaeleza washiriki hao muundo wa Tume hiyo kuwa unahusisha Mwenyekiti, Katibu, Wajumbe pamoja na Idara mbili na Vitengo saba vilivyoko ndani ya Tume.

Kwa upande wa Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya, Chitama alieleza kuwa Masula ya Walimu yanaamuliwa na Kamati ya Wilaya ambayo inaundwa na wajumbe mbalimbali huku Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya akiwa ndiye Katibu wa Kamati ya Wilaya na mtendaji mkuu wa Tume kwa ngazi ya Wilaya.

Na Mwandishi Wetu,
Dodoma.

# VIONGOZI TSC WAPATA CHANJO YA UVIKO-19

Baadhi ya Viongozi wa Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwemo Mwenyekekiti wa Tume hiyo Prof. Willy Lazaro Komba na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Mbena Nkwama, wameshiriki katika Uzinduzi wa Utoaji Chanzo ya UVIKO-19 kwa Mkoa wa Dodomauliofanyika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma Agosti 03, 2021.

Tukio hilo la utoaji wa chanjo lilizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Anthony Mtaka ambapo aliwataka wananchi wa Mkoa huo kuacha kuwa matomaso wa kwenye vitabu vya dini ili kuamini suala la chanjo ya UVIKO-19 na badala yake wajitokeze kuchanja katika maeneo katika maeneo yalitotengwa kwa ajili ya huduma hiyo.

Mtaka alisema Serikali imeona umuhimu wa kuagiza chanjo hiyo ili kuendelea kulinda afya za Watanzania, hivyo ni vizuri wananchi wa mkoa huo kutumia fursa hiyo ya kupata chanjo kama inavoelekezwa na wataalamu wa afya.

Pamoja na hilo Mhe. Mtaka amelielekeza Jeshi la Polisi mkoani Dodoma kuhakikishia wanasimamia utekelezaji wa abiria kukaa 'level seat' kwenye magari wakati wafanyabiashara kwenye masoko wakitoa huduma wakiwa wamevaa barakoa na menejimenti za masoko zikihakikisha kuwa kuna maji tiririka ya wananchi kunawa huku akiwaomba wamiliki wa vyombo vya usafiri kusaidia kama kuna uwezekano wa kupata barakoa basi wafanye hivyo ikiwa ni pamoja na kuepuka kubananisha watu katika maeneo ya biashara.

"Katika mazungumzo yangu na Jeshi la Polisi nimeelekeza pia tusiruhusu mishikaki kwa maana ya kupandisha abiria zaidi ya mmoja katika pikipiki moja na matumizi ya kofia za kujilinda na usalama katika



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba akipata Chanjo ya UVIKO-19 wakati wa uzinduzi wa Chanjo hiyo kwa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Agosti 3, 2021.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba akipokea cheti cha kuthibitisha kuwa amepata Chanjo ya UVIKO-19 wakati wa uzinduzi wa Chanjo hiyo kwa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Agosti 3, 2021.*

# VIONGOZI TSC WAPATA CHANJO YA UVIKO-19



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama, akipata Chanjo ya UVIKO-19 wakati wa uzinduzi wa Chanjo hiyo kwa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Agosti 3, 2021.*

pikipiki usiruhusiwe kwa zaidi ya mtu mmoja katika kipindi hiki cha ugonjwa, na badala yake kofia hizo zivaliwe na madereva wenyewe wa pikipiki walau kuwa tumesaidia sehemu moja ya kuepusha umbukizaji na usambaaji wa ugonjwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine." Alisema Mkuu wa Mkoa huyo.

Kwa upande wake Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akizungunza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Willy Komba kwa wananchi walioshiriki uzinduzi huo alishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan na Uongozi wa Mkoa kwa kuleta chanjo hizo na kuahidi kuendelea kuhamasisha walimu kujitokeza kupata chanjo hiyo kwa hiari.

"Sisi kama viongozi kwa hiari tumejitokeza ilikuhamasisha walimu nao kupata chanjo hii kwani walimu ni kundi kubwa katika utumishi wa umma na wanategemewa na kila fani katika Taifa lolote duniani. Hivyo, ni vema na wao wajitokeze kupata chanjo hii ili kulinda afya na kuendelea kutoa elimu kwa kada zote zinazowategemea kwa maendeleo ya Taifa". Alisema Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

Tukio hilo lilihudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Mkoa, Wilaya, Madhehebu mbalimbali, Vyama vya Siasa, Taasisi, Jumuiya na Wananchi wa Mkoa wa Dodoma na viunga vyake.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama, akionesha cheti cha kuthibitisha kuwa amepata Chanjo ya UVIKO-19 wakati wa uzinduzi wa Chanjo hiyo kwa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Agosti 3, 2021.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama, akitoa neno fupi wakati wa uzinduzi wa Chanjo ya UVIKO-19 kwa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Agosti 3, 2021.*

# MWELI ATAKA MIKOA, HALMASHAURI KUWA NA KANZIDATA ZA WADAU WANAOTOA HUDUMA YA ELIMUMSINGI

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Gerald Mweli amewataka Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuwa na kanzidata za wadau wanaosaidia katika kutoa huduma ya Elimumsingi katika maeneo yao.

Mweli ameyasema hayo wakati akifunga Kikao Kazi cha Asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma huku akiagiza kila Halmashauri iweke utaratibu wa kuwa na vikao walau vinne vya kukutana na wadau hao na kwa ngazi ya mkoa kufanya vikao viwili kwa mwaka.

Pamoja na hilo, Naibu Katibu Mkuu Mweli ameitaka mikoa yote kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa maelekezo hayo kila robo ya mwaka ili kuratibu ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wote wa Elimu kama sehemu ya utendaji wa pamoja wenye tija kwa Sekta ya Elimu na jamii kwa ujumla wake.

"Ufanisi wa wadau wa elimu unategemea sana ushirikiano wanaoupata kutoka Serikalini. Kutokana na ukweli huo, ni dhahiri kuwa wadau hawa wanatakiwa kuhudumiwa na kuelekezwa vizuri bila kusababisha vikwazo vya aina yoyote. Hivyo, viongozi wa Halmashauri na Mikoa endeleeni kushikamana na wadau katika kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali. Wasaidieni kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Miongozo, Kanuni na Taratibu bila kusababisha urasimu usio wa lazima." Alisema Naibu Katibu Mkuu Mweli

Alisema, kupitia kikao kazi hicho ameridhika na kuona umuhimu wa kila Asasi kufanya mapitio ya miradi yake (periodic review) na kuiwasilisha Serikalini kwa uelewa, utekelezaji na ufuatiliaji wa pamoja kwa maslahi ya watoto hapa nchini jambo ambalo litasaidia sio tu kutathmini ufanisi wa mradi bali pia kubaini changamoto zinazoweza kuathiri utelezaji wa miradi husika.

Naibu Katibu Mkuu Mweli aliongeza kuwa, katika kuunganisha nguvu na mikakati



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiwasilisha mada juu ya Maadili na Miiko ya kazi ya Ualimu katika kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi. Kikao kazi hicho kilichoandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kilifanyika Agosti 16-18, 2021 jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka TSC, Moses Chitama akijibu baadhi ya maswali ya washiriki wa kikao kazi kuhusu taratibu mbalimbali za utumishi wa umma katika kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi kilichofanyika jijini Dodoma.*

# MWELI ATAKA MIKOA, HALMASHAURI KUWA NA KANZIDATA ZA WADAU WANAOTOA HUDUMA YA ELIMUMSINGI



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo akitoa ufafanuzi juu ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016 katika kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya Walimu, Robert Lwikolela akitoa ufafanuzi juu ya Miiko na Maadili ya Utumishi wa walimu katika kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi kilichofanyika jijini Dodoma.*

ya utoaji wa elimu bora, mijadala ya kikao kazi hicho imedhihirisha kuwa sasa umefika wakati kuona umuhimu wa wadau kuandaa mipango na bajeti kwa kushirikisha Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kusaidia vipaumbele vitakavyotafsiri mahitaji muhimu na eneo mahususi la kufanyia kazi kwa wakati huo. Hivyo, kuelekeza kuwepo kwa ushirikiano wa karibu baina ya Serikali na asasi zote katika uandishi, upangaji na utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Sambamba na hilo, Mweli aliwataka viongozi wa ngazi ya Halmashauri na Mikoa kuhakisha wanalea na kusimamia asasi zote zilizomo katika maeneo yao na kuwapatia ushirikiano wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuratibu matumizi ya rasilimali zilizopo katika maeneo yao ili kuzipunguzia asasi hizo gharama za kiutawala.

Akitoa maelezo mafupi kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi kufunga kikao kazi hicho Mkurugenzi wa Usimamizi wa Elimu kutoka OR-TAMISEMI Bw. Ephraim Simbeye alisema asasi kama wadau wa elimu zimekuwa na mchango mkubwa katika kusaidiana na Serikali kutekeleza baadhi ya majukumu ambayo yanafanikisha azma ya utoaji wa elimu bora kwa wote.

"Baadhi ya asasi hizi zimejishughulisha na ujenzi wa madarasa, utoaji wa mafunzo kwa walimu, uanzishaji wa maktaba za shule, utoaji wa misaada ya kielimu kama taa zinazotumia mwanga wa jua, vitabu, madaftari, sare za shule, usafiri, taulo za kike na misaada mingine mingi kwa wanafunzi wanaotoka katika mazingira hatarishi, mazingira magumu kufikika, yatima, wenye mahitaji maalum na kaya maskini." Alisema Simbeye.

Aliongeza kuwa zipo asasi zinazoboresha ufundishaji na ujifunzaji darasani kwa njia ya TEHAMA, kutoa mafunzo ya kuwajengea walimu uwezo katika ufundishaji, kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto hususani wa kike ili waweze kumaliza mzunguko wao wa Elimu baada ya kuandikishwa shule.

Aidha, Simbeye alibainisha kuwa pamoja na utekelezaji wa majukumu hayo ya kielimu, kuna changamoto zilizobainika kutokana na utekelezaji wa shughuli za wadau ambazo ni pamoja na; kuwepo kwa baadhi ya mikoa ambayo ina asasi chache

# MWELI ATAKA MIKOA, HALMASHAURI KUWA NA KANZIDATA ZA WADAU WANAOTOA HUDUMA YA ELIMUMSINGI




*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi wakiwa kwenye kikao.*

zinazotekeleza shughuli za kielimu akitolea mfano wa mikoa ya Katavi, Tabora, Shinyanga na katika baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Rukwa; kuwepo kwa asasi zinazotekeleza shughuli zinazofanana katika eneo moja kupitia mbinu zinazotofautiana kwa ubora; baadhi ya wadau kutojitambulisha katika ngazi ya mkoa na mikoa kutokuwa na utaratibu wa kuratibu utendaji kazi wa asasi hizo; baadhi ya asasi kukwamishwa katika utendaji kazi kutokana na urasimu na kutokufuatwa kwa taratibu za mawasiliano katika ngazi tofauti; na baadhi ya miradi iliyoanzishwa na wadau kutoendelezwa baada ya miradi hiyo kufikia tamati, akitolea mfano wa majengo yanayojengwa kutokarabatiwa.

Nae Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama, akiwasilisha mada kuhusiana na Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu alisisitiza kuwa moja ya eneo linalohitaji nguvu ya pamoja na wadau mbalimbali ni utafiti, ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015, TSC ina jukumu la kufanya tafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa walimu na kumshauri Waziri inavyostahiki.

"TSC bado haijafanya vizuri sana kwenye eneo hili la utafiti kutokana na ufinyu wa bajeti. Lakini sote tunakubaliana kuwa suala la utafiti ni jambo muhimu sana katika maendeleo ya walimu wetu na elimu kwa ujumla wake hapa nchini. Hivyo, tunawakaribisha wadau wetu mje tushirikiane tufanye tafiti zenye tija kwa Taifa na kwa maslahi ya walimu na wanafunzi wetu," aliongeza Nkwama.

Katika kikao kazi hicho kilichoandaliwa wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Nkwama aliambatana na Maafisa waandamizi kutoka TSC ambao walipata fursa ya kufafanua masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu.



*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi kilichohusisha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la Elimumsingi wakiwa kwenye kikako.*

# TSC MBIONI KUJENGA OFISI ZAKE DODOMA



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kulia) akiongea na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba wakati walipotembelea kiwanja cha Tume hiyo kilichopo eneo la Chinyoyo jijini Dodoma Agosti 24, 2021. TSC inatarajia kuanza ujenzi wa jengo la ofisi yake katika eneo hilo hivi karibuni.*

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Utumishi wa walimu (TSC) iko mbioni kuanza ujenzi wa ofisi zake za Makao Makuu katika eneo la Chinyoyo lililopo jijini Dodoma baada ya kununua kiwanja katika eneo hilo kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma.

Agosti 24, 2021 Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akiwa pamoja na Katibu wa Tume hiyo, Paulina Nkwama walitembelea eneo hilo la mradi wa ujenzi wa ofisi kwa ajili ya kukagua na kujiridhisha na mipaka ya kiwanja kabla ya taratibu za ujenzi kuanza.

Wakiwa katika eneo hilo, viongozi hao walionesha kuridhishwa na jiografia ya eneo la mradi wa ujenzi ambalo tayari lilikuwa limewekewa alama za mipaka huku wakieleza kuwa mara baada ya taratibu kukamilika utekelezaji wa mradi huo utaanza mara moja.

Hatua ya TSC kumiliki eneo hilo ni moja ya jitihada za maksudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuendeleza ujenzi wa Ofisi za Umma katika Makao Makuu ya Nchi, Dodoma.

TSC inatarajia kuanza kutekeleza mradi huo kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) huku ikiwa imetengewa kiasi cha shilingi milioni mia tano katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ambazo ni gharama za awali za ujenzi huo.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kushoto) akimwonesha Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba mipaka ya kiwanja cha Tume kilichopo kitalu AA eneo la Chinyoyo Jijini Dodoma chenye ukubwa wa mita za mraba 3,348.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba wa (wa kwanza mwenye miwani) akiongea jambo na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakati walipotembelea kiwanja cha Tume kilichopo kitalu AA eneo la Chinyoyo Jijini Dodoma hivi karibuni. Wengine ni watumishi wa TSC walioambatana na viongozi wa hao.*




*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa TSC, Lameck Mbeya (kushoto) akitoa maelezo kwa Katibu wa TSC na watumishi wengine waliotembelea kiwanja cha TSC kilichopo eneo la Chinyoyo jijini Dodoma Agosti 24, 2021.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiwa pamoja na baadhi ya watumishi wa Tume hiyo wakiangalia kiwanja cha TSC ambacho ndipo zinapotarajiwa kujengwa ofisi za makao makuu ya Tume hiyo.*



*Mwenekano wa Kiwanja Na.939, Kitalu AA kilicopo eneo la Chinyoyo Jijini Dodoma chenye ukubwa wa mita za mraba 3,348 ambacho kinamilikiwa na TSC.*



*Mwenekano wa Kiwanja Na.939, Kitalu AA kilichopo eneo la Chinyoyo Jijini Dodoma chenye ukubwa wa mita za mraba 3,348 ambacho kinamilikiwa na TSC.*

# RC MTAKA AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA MAADILI YA WALIMU

Na Mwandishi Wetu

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kufanya kazi kwa bidii katika kuwahudumia walimu wa shule za msingi na sekondari katika masuala ya Maadili na Nidhamu.

Mtaka alitoa pongezi hizo hivi karibuni wakati akifunga kongamano la siku mbili la walimu wenye mahitaji maalum lililoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na kuhudhuriwa na wawakili wa walimu hao kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara.




*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka akitoa hotuba ya kufunga Kongamano la walimu wenye ulemavu kutoka Wilaya za Tanzania Bara lililofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Pichani upande wa kushoto ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama na katikati ni Makamu wa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Dinah Mathamani.*




*Makamu wa Rais wa Chama wa Walimu Tanzania (CWT), Dinah Mathamani akiongea na walimu waliohudhuria Kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Pembeni yake ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kushoto) akiongea jambo na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama wakati wa Kongamano la walimu wenye ulemavu Tanzania Bara lililofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# RC MTAKA AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA MAADILI YA WALIMU

Alisema kuwa kutokana na juhudi zinazofanywa na TSC, kumekuwa na mabadiliko chanya kwa walimu kuzingatia taratibu za utumishi wao kitu ambacho kimesaidia kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari.

"Pamoja na kwamba yapo matukio ya hapa na pale ya utovu wa nidhamu kwa walimu wachache, ninakiri kwamba TSC mmefanya kazi kubwa katika kujenga nidhamu na maadili kwa walimu wetu. Siku hizi kumekuwa na utulivu mkubwa tofauti na siku za nyuma, hii haina maana kuwa changamoto za walimu zimekwisha kabisa lakini mmewaelekeza namna ya kushughulikia mambo yao bila kukiuka taratibu za utumishi," alisema Mtaka.

Mtaka aliongeza kuwa ili walimu waweze kufanya kazi vizuri ni lazima mamlaka zenye dhamana na usimamizi wa sekta hiyo kuhakikisha walimu wanaandaliwa vizuri na pale wanapoingia kwenye utumishi ni lazima watunzwe vizuri ili wapate hamasa ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi.

"Katibu TSC nakupongeza sana kwa uchapakazi wako mzuri ambao umesababisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kukuteua wewe katikati ya wengi ili uiongoze Tume. Ni imani yangu kuwa una mikakati mingi ya kuwasaidia walimu ili tuendelee kuona matokeo mazuri ya wanafunzi wetu. Binafsi ninaamini kwamba ili upate matokeo mazuri ya ufaulu kwa wanafunzi ni lazima walimu wawe wanaandaliwa na kutunzwa vizuri katika utumishi wao, "alisema Mkuu wa Mkoa.

Mkuu wa Mkoa huyo alisisitiza kuwa pale walimu wanapofanya vizuri ni vyema kuwe na utaratibu wa kutambua juhudi hizo ili kuwatia chachu wengine kufanya vizuri huku akieleza kuwa walimu wasipotambuliwa katika juhudi zao ni rahisi kuvunjika moyo na kukata tamaa.

"Nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu nilikuwa nimeweka utaratibu wa kuwapa motisha walimu waliokuwa wanafanya



*Baadhi ya Walimu wakiwa katika kongamano la walimu wenye ulemavu lililofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# RC MTAKA AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA MAADILI YA WALIMU

vizuri kwa kufaulisha wanafunzi. Kwa kweli wote tulishuhudia mabadiliko makubwa ya kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa Mkoa ule kutokana na morali waliyokuwa nayo walimu", alisisitiza.

Pamoja na hayo, Mtaka alieleza kuwa TSC haipaswi kufumbia macho uvunjifu wa maadili unaofanywa na baadhi ya walimu kwani watumishi wa umma wakiwemo walimu wana miiko na maadili ya kazi zao huku akitaja makosa ya utoro na uhusiano wa mapenzi na wanafunzi kuwa bado yanaonekana kushamiri kwa baadhi ya walimu.

Aliishauri TSC kukaa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na kuwaonesha mashauri mbalimbali ya walimu na namna yalivyoamuliwa ili CWT waone picha halisi ya hali ya walimu ilivyo lengo likiwa ni kuongeza juhudi katika kutoa elimu kwa walimu.

"Ni vizuri TSC mtafute muda mkae na CWT muwaoneshe kesi za walimu na kama mmewafukuza muwaeleze hali halisi. Na nyie CWT mkienda kwa walimu muwaeleze kwa uwazi kuwa wapo wenzenu ambao tabia zao hazivumiliki na wamefukuzwa kazi", alisema Mkuu wa Mkoa.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa huyo alishauri CWT kujitokeza na kuwatetea walimu wao pale wanapokabiliwa na mashuri ya nidhamu kwa kuwa wapo wengine wanajikuta wanaadhibiwa kutokana na kushindwa kujitetea vizuri kwa kuwa hawana uelewa wa mambo ya sheria.

"CWT ni lazima muangalie maslahi ya walimu wenu, wakati mwingine unaweza kukuta mwalimu ameshtakiwa lakini pengine alikuwa na sababu nzuri tu ambazo zinatosha kumuondolea hatia lakini kutokana na kukosa uelewa unakuta anafukuzwa kazi. Kama mkisimama vizuri mtaweza kuwasaidia wale wanaofaa kusaidiwa," alisema Mtaka.

Katika Kongamano hilo Katibu wa TSC, Paulina Nkwama aliambatana na viongozi waandamizi wa Tume ambapo walipata fursa ya kuwasilisha mada mbalimbali zilizohusu utumishi wa walimu.



*Baadhi ya Walimu wakiwa katika kongamano la walimu wenye ulemavu lililofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# ASASI MBALIMBALI NCHINI KUENDELEA KUUNGANA NA SERIKALI KATIKA KUBORESHA MAZINGIRA YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KATIKA KUTEKELEZA SERA YA ELIMU BILA MALIPO

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli amezitaka asasi mbalimbali hapa nchini kuendelea kuungana na Serikali katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika kutekeleza Sera ya Elimu Bila Malipo, ambayo imekua ikiongeza udahili wa wanafunzi mwaka hadi mwaka kwa kila ngazi ya elimu hali inayosababisha changamoto ya miundombinu hasa madarasa, madawati na vyoo.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli akifunga kikao kazi cha siku tatu cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika jijini Dodoma.

"Kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga Kidato cha Kwanza mwaka 2022 ni wazi kutakuwa na upungufu wa madarasa na madawati hivyo kuiomba kila asasi iunge mkono juhudi za Serikali katika maandalizi ya kuwapokea wanafunzi hawa kwa kuchangia ujenzi na ukarabati wa miundombinu hasa madarasa, vyoo na madawati katika maeneo wanayofanyia kazi wakati utaratibu utakaowezesha kila mdau kutekeleza suala hilo ukiandaliwa." Alisema Naibu katibu Mkuu (Elimu), Mweli.

Pamoja na hilo, Mweli alitoa wito kwa asasi zisizo za Kiserikali kujitokeza kusaidiana na Serikali katika kutatua changamoto ya uwepo wa watu wazima au watoto ambao hawajui kusoma na kuandika kwani Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni muhimu kuimarishwa.

Nae Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama, akiwasilisha mada kuhusiana na Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu alisema ili kujenga Taifa lenye watu waadilifu na lenye maendeleo, walimu wanalo




*Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli (mwenye tai nyekundu) akitembelea moja ya banda la washiriki wa kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli (mwenye tai nyekundu) akitembelea moja ya banda la washiriki wa kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# ASASI MBALIMBALI NCHINI KUENDELEA KUUNGANA NA SERIKALI KATIKA KUBORESHA MAZINGIRA YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KATIKA KUTEKELEZA SERA YA ELIMU BILA MALIPO

jukumu kubwa la kuhakikisha wanakuwa waadilifu.

Alisema uzingatiaji wa maadili na miiko ya ualimu utasaidia kuifanya kazi ya Ualimu iendelee kuheshimiwa na kuweza kuandaa viongozi wenye weledi kwani wataalam wote hupitia mikononi mwa walimu na hii itasaidia kuwa na Taifa lenye watu waadilifu na nchi iendelee kuwa yenye amani na utulivu.

Akielezea kwa ufupi historia ya usimamizi wa utumishi wa walimu Mwl. Nkwama alisema katika nchi yetu utumishi wa walimu umepitia katika hatua mbalimbali tangu uhuru, awali walimu walikuwa chini ya waajiri tofauti tofauti waliokuwa na masharti tofauti ya ajira na baadhi ya masharti ya ajira chini ya waajiri wengine, yalikuwa yakiwanyima walimu haki zao za msingi, lakini pia kulikuwa na tofauti ya maslahi kati ya walimu wenye sifa zinazolingana kutegemeana na mwajiri ambao walikuwa ni Serikali, Mashirika/ Madhehebu ya Dini na binafsi.

Katibu wa TSC aliendelea kusisitiza kuwa walimu wamekabidhiwa watoto wakati wawapo shuleni kwani ndilo eneo ambalo watoto hukaa kwa kipindi kirefu zaidi nyakati za mchana na hivyo wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla wanategemea matunzo ya hali ya juu ya watoto, kufundishwa kwao vema, na




*Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli (mwenye tai nyekundu) akiwa katika picha ya pamoja na wadau mbalimbali walioshiriki kiako kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Kushoto kwa Naibu Katibu huyo ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama.*




*Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli (mwenye tai nyekundu) akiwa katika picha ya pamoja na wadau mbalimbali walioshiriki kiako kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Kushoto kwa Naibu Katibu huyo ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama.*

# ASASI MBALIMBALI NCHINI KUENDELEA KUUNGANA NA SERIKALI KATIKA KUBORESHA MAZINGIRA YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KATIKA KUTEKELEZA SERA YA ELIMU BILA MALIPO

kulelewa vizuri kimaadili kwa kuzingatia nguzo za maadili ya kazi ya ualimu ili kuwa raia wema wa baadaye.

Alizitaja nguzo hizo za maadili ya kazi ya ualimu kuwa ni pamoja na; kumlea mtoto Kimwili (kwa maana ya kutomdhuru, mazingira safi na salama ya shule na usafi wa mwili; Kiakili (Maarifa na Ujuzi); Kiroho (Heshima, Huruma, Msamaha na Kuhimiza kuhudhuria Vipindi vya Dini); Kijamii - Kushirikiana (wao kwa wao na Jamii), Kuvumiliana, Kusaidiana, kushiriki michezo na kazi shuleni.

Mwl. Nkwama alibainisha kuwa mwalimu ameajiriwa kwa kazi ya kufundisha watoto/ wanafunzi na hivyo ili awe mwalimu mzuri anayewajibika vizuri ni lazima; Aipende kazi yake ya ualimu, Azingatie kwa hali ya juu maadili ya kazi yake na kuitetea, Afanye kazi yake kwa bidii na kwa kujituma, Awe mbunifu, Ahakikishe anainua kiwango chake cha elimu na cha utendaji kazi wakati wote, Asitumie madaraka yake vibaya na awe mfano bora wa kuigwa na wanafunzi.

Mwisho, Katibu wa Tume Mwl. Nkwama aliongeza kwa kusema kuwa wajibu wa mwalimu yeyote katika Taifa lake anatakiwa kuwa mzalendo safi na raia mwema na mtii wa Sheria za nchi na mwelekezaji wa wanafunzi kuwa wazalendo safi na raia wema wa baadaye kwani nguzo hii inamtaka mwalimu aipende nchi yake kwa moyo wake wote, awe na uelewa wa Sheria za nchi na kuzitii, asitende matendo ya kihalifu na awe mfano bora kwa jamii na watoto/ wanafunzi shuleni na nje ya eneo la shule.

Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers' Service Commission - TSC) ilianzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hiyo na Kanuni zake za mwaka 2016. Aidha, Tume ilianza kutekeleza majukumu yake rasmi katika kipindi cha mwaka fedha 2016/17 ikiwa ni Mamlaka ya Ajira (Appointing Authority) na Nidhamu (Disciplinary Authority) kwa Walimu wote wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma.




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (mwenye barakoa nyeupe) akibadilishana mawazo na baadhi ya wadau walioshiriki kiako kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# SUMA JKT WATEMBELEA ENEO LA MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA TSC



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akionesha alama ya mpaka wa kiwanja cha TSC wakati wa ziara ya wataalamu wa ujenzi kutoka Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) katika eneo la Chinyoyo jijini Dodoma iliyofanyika Juni 25, 2021.*



*Mhandisi Tendwa Mahunnah kutoka SUMA JKT akitoa maelezo kwa Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (katikati mwenye miwani) kuhusu ramani ya kiwanja cha TSC wakati timu ya wahandisi kutoka SUMA JKT pamoja na TAMISEMI walipotembelea eneo la mradi wa ujenzi wa ofisi za TSC Makao Makuu. Wengine ni watumishi wa TSC waliokuwa kwenye ziara hiyo.*

**Na Mwandishi Wetu**

Wataalamu wa ujenzi kutoka Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wametembelea kiwanja cha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichopo eneo la Chinyoyo jijini Dodoma kwa lengo la kufanya tathmini ya eneo hilo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ofisi za Tume Makao Makuu.

Mara baada ya kuwasili katika eneo hilo, wahandisi hao ambao waliambatana na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama pamoja na watumishi wa Tume hiyo walianza kukagua alama za mipaka ya eneo ili kujiridhisha kama inaendana na ramani ya kiwanja hicho.

Baada ya uhakiki wa mipaka



*Wataalamu wa ujenzi wakipiga picha alama za mipaka ya kiwanja cha TSC ikiwa ni sehemu ya kukamilisha taratibu za awali kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ofisi hizo.*



*Mhandisi Tendwa Mahunnah kutoka SUMA JKT akionesha sehemu itakayowekwa lango la kuingilia mara baada ya jengo la TSC litakapojengwa katika eneo Chinyoyo jijini Dodoma.*

# SUMA JKT WATEMBELEA ENEO LA MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA TSC



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akisoma ramani ya kiwanja cha TSC kilichopo eneo la Chinyoyo jijini Dodoma. Pichani, upande wa kushoto ni Afisa Tawala Mkuu kutoka TSC, Omar Ilyas na upande wa kulia ni Mhandishi Tendwa Mahunnah kutoka SUMA JKT.*



*Afisa Tawala Mkuu kutoka TSC, Omar Ilyas (mwenye barakoa) akisikiliza jambo kutoka kwa Mhandisi Tendwa Mahunnah kutoka SUMA JKT wakati wa ziara ya wataalamu hao katika kiwanja cha TSC kilichopo eneo la Chinyoyo, Dodoma.*

ya kiwanja hicho, wahandisi hao walimuonesha Katibu wa Tume pamoja na timu yake namna jengo hilo litakavyokaa katika kiwanja hicho ikiwa ni pamoja na jiografia ya sehemu za kuingilia, sehemu za maegesho ya magari pamoja maeneo mengine ya ofisi hiyo.

Wataalamu hao walioneshwa kuridhishwa na eneo hilo na kueleza kuwa mchoro wa jengo hilo umezingatia vitu vyote muhimu na kuahidi kuwa pale taratibu zitakapokamilika mradi huo utaanza kutekelezwa mara moja.

Kwa upande wake, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama aliwashukuru wahandisi hao kwa kufanya ziara katika eneo hilo na kueleza kuwa hatua hiyo inasaidia kuwa na uelewa wa pamoja kati ya mkandarasi na mteja jambo ambalo litaleta tija wakati wa ujenzi.



*Watumishi wa TSC, Francis Gwankisa (kushoto) pamoja na Jumanne Muhitila wakifurahia jambo katika kiwanja cha TSC kilichopo eneo la Chinyoyo Dodoma ambapo ndipo zitakapojengwa ofisi za TSC Makao Makuu.*

Aliongeza kuwa taratibu za utekelezaji wa mradi huo zinaendelea vizuri na TSC inatarajia kuwa pale ujenzi utakapoanza, mkandarasi huyo ambaye ni SUMA JKT atafanya kazi yake vizuri kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusika ili kuhakikisha miradi ya Serikali inaendelea kufanyika kwa ubora unaohitajika.

Katika mradi huo, wataalamu wa masuala ya ujenzi kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI wanashirikiana kwa karibu na TSC ili kutoa ushauri wa kitaalamu unaohitajika katika ujenzi wa jengo hilo linalotarajiwa kuanza kujengwa hivi karibuni.

# ZOEZI LA UBAINISHAJI WA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUMU LIMEKUWA NA MAFANIKIO MAKUBWA MWAKA 2021 IKILINGANISHWA NA MWAKA 2018 – MWELI

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli amesema zoezi la ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu ambalo limefanyika katika kipindi cha mwaka 2021 limekuwa na mafanikio makubwa ukilinganisha na zoezi la mwaka 2018.

Akizungumza wakati wa kufunga kikao kazi cha siku tatu cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika jijini Dodoma Mweli alieleza kuwa Kata zilizofikiwa katika kuwabaini watoto hao zimeongezeka kutoka 2,723 mwaka 2018 hadi kata 3,785 mwaka 2021 huku idadi ya watoto waliojitokeza imeongezeka kutoka watoto 29,804 hadi watoto 59,784 na idadi ya watoto waliobainika kuwa na mahitaji maalumu imeongezeka kutoka 16,463 mwaka 2018 hadi kufikia 28,698 mwaka 2021.

Alisema, "matokeo ya zoezi hilo yamefanikisha kutambua watoto wenye mahitaji maalumu na hivyo kutokana na taarifa hizi, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa elimu, itaweza kupanga mipango sahihi ya kuwapatia afua stahiki kwa urahisi."

Naibu Katibu Mkuu Mweli alisema, Serikali inatekeleza na kusimamia eneo la Elimu Jumuishi kwa kuzingatia Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa Miaka Mitatu (2018/2021) yaani National Strategy for Inclusive Education – NSIE (2018/2021) ulioandaliwa na kusisitiza wadau wa elimu maalumu/ jumuishi nchini kuendelea kuzingatia vipaumbele vya kitaifa vilivyoainishwa katika mkakati huo.

Aidha alisema, baadhi ya wadau wamelalamikia hali ya utunzaji na uendelezaji wa miundombinu inayojengwa katika Halmashauri huku katika mazingira mengine jamii kutoonesha umiliki wa miradi na hivyo miradi hiyo kushindwa kudumu wakati asasi iliyoianzisha inapoikabidhi Serikalini.

"Kutokana na hali hiyo, ninazielekeza Halmashauri zote kuweka mkakati wa kuhakikisha wanatunza na kulinda miradi yote inayoanzishwa na wadau wakati huohuo jamii ikihusishwa katika uanzishwaji na uendelezaji wa miradi hiyo ili waione miradi hiyo kuwa yao na sio miradi ya wafadhiri." Alisema Mweli.

Naibu Katibu Mkuu Mweli, alizishukuru na kuzipongeza asasi zote zilizoshiriki pamoja na Serikali kwa kuitikia wito na kudhamini Kikao Kazi hicho ikiwa ni pamoja na; Children in Crossfire (CiC), Project Concern International (PCI), Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Light for the World, Aga Khan Foundation (AKF), Data Vision Tanzania, World Education Inc., Social Action Trust Fund (SATF), Research Triangle Institute (RTI), na Young Scientists kwani huo ni mwanzo wa ushirikiano kwa maendeleo ya watoto na Taifa kwa ujumla.

Nae Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama, akiwasilisha mada kuhusiana na Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu alisema baadhi ya makosa ya kinidhamu yanayofanywa na walimu mara kwa mara yanatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufinyu wa upatikanaji wa fursa za kujengeana uwezo kwa kupeana elimu ya mara kwa mara katika eneo la Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu baada ya ajira na wakati wa utumishi wao baada ya kutoka vyuoni jambo ambalo linahitaji ushirikiano na wadau mbalimbali wa elimu nchini.

"Baadhi ya makosa yanayofanywa na walimu wetu hapa nchini ni pamoja na; utoro kazini unaotokana na kuondoka kituoni bila kuwa na ruhusa ya mwajiri, kujiongezea muda wa ruhusa, kuzidisha siku za likizo au kuacha kazi bila kufuata utaratibu wa kiutumishi." Alisema Mwalimu Nkwama.

Aliyataja makosa mengine kuwa ni kukataa uhamisho, kutotii mamlaka, kumsababishia mwajiri hasara/ kuharibu mali, kuwa na uhusiano wa kimapenzi/ kubaka/ kulawiti wanafunzi, kuchelewa kazini au kuondoka kituoni wakati wa muda wa kazi bila ruhusa ya Mkuu wa Shule/ Mwalimu Mkuu pamoja na ulevi.

Nkwama aliendelea kueleza kuwa makosa mengine ni uzembe kazini kwa kutokuandaa masomo, kutofundisha, kutotunga mitihani na kusahihisha kazi za wanafunzi au mitihani, kashfa za mitihani, kukaririsha wanafunzi bila kibali cha mamlaka, kutumia vibaya madaraka na makosa ya jinai.

Kikao hicho kilishirikisha washiriki wapatao 400 wakiwemo wawakilishi wa Asasi mbalimbali zinazojishughulisha na Elimu nchini, viongozi wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, OR-TAMISEMI, Wawakilishi wa Maafisa Elimu Mikoa ya Tanzania Bara na Tume ya Utumishi wa Walimu.

# UTOAJI VIBALI VYA UTEKELEZAJI MIRADI YA AFUA ZA ELIMU MSINGI KULENGA MIKOA NA HALMASHAURI AMBAZO HAZINA WADAU

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli amesema utoaji wa vibali vya utekelezaji wa afua mbalimbali za wadau katika miradi yao mipya uzingatie maelekezo ya Serikali yanayohitaji miradi hiyo hapa nchini kuelekezwa na kutekelezwa zaidi katika Halmshauri ambazo hazina wadau au zenye wadau wachache kutokana na mtawanyiko wa wadau wa Elimumsingi katika Mikoa na Halmashauri nchini kuwa na uwiano usio sawa.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli akifunga kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu msingi kilichofanyika jijini Dodoma.



*Washiriki wa kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao kikiendelea.*



*Washiriki wa kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao kikiendelea.*

"Kama mlivyoona kwenye ramani mtawanyiko wa wadau wa Elimumsingi katika Mikoa na Halmashauri nchini hauna uwiano sawa. Mathalani, halmashauri ishirini na tisa (29) hazina mdau hata mmoja wakati kuna halmshauri sita (6) zenye wadau zaidi ya kumi na tano (15). Kwa upande wa mikoa, mikoa mitano (5) ina wadau chini ya kumi (10) wakati mikoa mitatu tu ina wadau zaidi ya sitini na tano (65) na kuna mkoa mmoja una wadau themanini na tatu (83). Mtawanyiko huu usio sawa wa wadau unachangia ongezeko la

# UTOAJI VIBALI VYA UTEKELEZAJI MIRADI YA AFUA ZA ELIMU MSINGI KULENGA MIKOA NA HALMASHAURI AMBAZO HAZINA WADAU

tofauti ya ubora wa Elimu Kimkoa na Halmashauri." Alisema Naibu Katibu Mkuu (Elimu).

Naibu Katibu Mkuu Mweli akifafanua alisema, uhalisia wa kiutendaji unaonesha kuwa asasi nyingi zimekuwa zikifanya shughuli zake nje ya mfumo wa kiutawala wa Serikali na hivyo kushauri kwakuwa Serikali ina watendaji na viongozi katika ngazi zote ni vema asasi zione umuhimu wa kutumia rasimali hizo kutekeleza afua zao katika eneo husika.

"Ili kuongeza ufanisi, shirikianeni na Serikali kwa rasilimali zilizopo ili kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi na hivyo kuongeza wigo wa wanufaika wa afua hizo. Hali kadhalika imeonekana kuna asasi ambazo zinatoa afua za aina moja katika sehemu moja. Ili kuongeza ufanisi ninashauri asasi hizo kuangalia namna ya kuingia ubia miongoni mwao ili kujengeana uwezo na kupunguza gharama za utoaji wa afua hizo. Hii pia itasaidia kujua nani yuko wapi na anafanya nini kwani asasi itapewa kibali na OR-TAMISEMI". Aliongeza Mweli.

Alisema, shughuli zote za asasi sharti ziendeshwe kwa kuzingatia Sheria, Miongozo na Kanuni kuhusu usimamizi wa elimu nchini jambo ambalo limeonesha uhitaji wa kutengeneza mwongozo wa uratibu wa wadau wa elimu akiongeza kuwa mwongozo huo pamoja na mambo mengine utabainisha aina za afua ambazo wadau wanaweza kuzitekeleza kwa kupata vibali katika Halmashauri husika au katika ngazi ya Mkoa.

Wakati huohuo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama alieleza kuwa pamoja na kwamba



*Washiriki wa kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao kikiendelea.*

# UTOAJI VIBALI VYA UTEKELEZAJI MIRADI YA AFUA ZA ELIMU MSINGI KULENGA MIKOA NA HALMASHAURI AMBAZO HAZINA WADAU

Serikali kupitia TSC imefanya kazi kubwa katika kutoa huduma kwa walimu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu na. 25 ya mwaka 2015, bado milango iko wazi kwa wadau mbalimbali wanaopenda kushirikiana na Tume hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.

"Serikali imefanya kazi kubwa katika kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu nchini, hata hivyo tunaona kuwa yapo maeneo ambayo tunapaswa kuongeza nguvu zaidi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuwasaidia walimu waweze kutimiza majukumu yao ya kuwafundisha wanafunzi kikamilifu," alisema Nkwama.

Aidha, alifafanua kuwa walimu wengi bado hawajawa na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa kuzingatia miiko na maadili ya kazi yao ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma, kitu ambacho kinasababisha baadhi yao kuingia katika makosa ya kinidhamu bila wao wenyewe kujua.

"Kwenye eneo hili tunapaswa kuongeza nguvu katika kuwafikia walimu na kuwakumbusha Sheria, Kanuni na Taratibu za Kiutumishi. Hivyo, tunawakaribisha wadau wote wanaopenda tushirikiane kwa pamoja katika kutoa elimu kwa walimu wetu ili wajiepushe na makosa ambayo yanasababisha wachukuliwe hatua mbalimbali za nidhamu ikiwemo kufukuzwa kazi", alifafanua Nkwama.

Kikao hicho kilishirikisha washiriki wapatao 400 wakiwemo wawakilishi wa Asasi mbalimbali zinazojishughulisha na Elimu nchini, viongozi wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, OR-TAMISEMI, Wawakilishi wa Maafisa Elimu Mikoa ya Tanzania Bara na Tume ya Utumishi wa Walimu.



*Washiriki wa kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao kikiendelea.*

# TUGHE TAWI LA TSC WAFANYA UCHAGUZI WA VIONGOZI



*Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Francis Gwankisa akitoa neno la shukrani baada ya uchaguzi wa viongozi wa tawi hilo kukamilika na yeye kuchaguliwa katika nafasi ya Mwenyekiti wa Tawi. Pembeni yake ni Katibu Mpya wa Tawi hilo, Enid Geofrey. Uchaguzi huo ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma, Agosti 27, 2021.*

**Na Mwandishi Wetu.**

Wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamefanya uchaguzi wa viongozi wake baada ya viongozi waliokuwepo kumaliza muda wao kwa mujibu wa katiba ya chama hicho.

Uchaguzi huo uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Agosti 27, 2021 ulisimamiwa na Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma, Anter Tarimo ambaye aliwataka wagombea na wanachama wote kuzingatia na kuheshimu taratibu za uchaguzi ili zoezi hilo lifanyike kwa ufanisi.

Akieleza utaratibu wa uchaguzi huo, Tarimo alisema kila mgombea ana haki ya kupata nafasi ya kujinadi na kuomba kura, wapiga kura watauliza maswali na mgombea atajibu, kisha zitatolewa karatasi maalum ambazo wapiga kura watazitumia kupiga kura.

Aliendelea kufafanua kuwa baada ya kupiga kura karatasi zote zitakusanywa kwa utaratibu maalum na kila mgombea atachagua mwakilishi wake ambaye atashuhudia kura zikihesabiwa na kisha wagombea watapaswa kusaini fomu za kukubali matokeo.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa Katiba ya TUGHE nafasi zinazogombewa ni Mwenyekiti wa Tawi, Katibu wa Tawi, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake, Katibu Kamati ya Wanawake, Mweka



*Baadhi ya wanachama wa TUGHE Tawi la TSC wakiwa katika kikao cha uchaguzi wa viongozi wa tawi hilo.*

# TUGHE TAWI LA TSC WAFANYA UCHAGUZI WA VIONGOZI



*Kikao cha uchaguzi wa viongozi wa TUGHE Tawi la TSC kikiwa kinaendelea.*

Hazina wa Kamati ya Wanawake Pamoja na Wajumbe nane wa Tawi.

Baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika, Tarimo alitangaza matokeo ambapo alieleza kuwa washindi katika nafasi zilizokuwa zinagombewa ni Francis Gwankisa (Mwenyekiti wa Tawi), Enidi Geogrey (Katibu wa Tawi) pamoja na wajumbe wa kamati ya Tawi ambao ni Mashaka Athumani, Timoth Mtafya, Laila Bhai, Catherine Kamili, Rajab Kalobo, Judith Mbuki, Bitwalihati Magota, na Josephine Kabisi.

Kwa upande wa Kamati ya Wanawake, waliochaguliwa ni Waeli Chaki (Mwenyekiti), Flora Chanda (Katibu), Happy Jumapili (Mweka Hazina) na wajumbe wa kamati hiyo ni Sophia Kutona pamoja na Nelusiwe Kajegela.

Akitoa neno la shukrani, Mwenyekiti mpya wa TUGHE ambaye pia ni Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Francis Gwankisa aliwashukuru wanachama wote kwa kuonesha imani kwake kwa kumchagua yeye Pamoja na wenzake kuongoza chama hicho kwa kipindi cha miaka mitano.

"Ninashukuru sana kwa imani na heshima kubwa ambayo mmenionesha mimi binafsi pamoja na wenzangu wote ambao tumechaguliwa leo, ninaahidi kuwa tutafanya kazi kwa bidii, weledi na maarifa na pia tutashirikiana nanyi kwa kila namna katika kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu haki na maslahi ya watumishi wote wa Tume," alisema Gwankisa.



*Afisa Tawala Mkuu kutoka Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Omar Ilyas (kushoto) akiwa pamoja na Afisa Utumishi, Judith Mtalai wakati wa kikao cha uchaguzi wa TUGHE Tawi la TSC Agosti 27, 2021.*

# TUGHE TAWI LA TSC WAFANYA UCHAGUZI WA VIONGOZI



*Wanachama wa TUGHE Tawi la TSC, Timoth Mtafya (kulia), Josephine Kabisi (katikati) na Grace Mauki (kushoto) wakiwa katika kikao cha uchaguzi wa viongozi wa chama hicho uliofanyika Agosti 27, 2021.*

Pamoja na shukrani hizo, Gwankisa alisema kuwa tawi hilo linakabiliwa na changamoto ya idadi ndogo ya wanachama ikilinganishwa na idadi ya watumishi wote waliopo TSC huku akiweka wazi kuwa jukumu lililopo mbele yao ni kutoa elimu kwa watumishi wa Tume hiyo ili waweze kujiunga na Chama hicho.

"Tukiangalia idadi ya wanachama wa TUGHE tawi la TSC hawazidi 35 lakini watumishi wote tupo zaidi ya 500. Kazi kubwa tuliyonayo ni kuimarisha chama kwa kuhakikisha watumishi wote wa TSC wanajiunga na TUGHE, hatuwezi kuwalazimisha kujiunga bali tunapaswa kuwaonesha faida za kujiunga hapa badala ya kuendelea kuwa kwenye vyama vingine wakati hawafanyi kazi tena huko walipokuwa mwanzo," alisema Gwankisa.

Aidha, Gwankisa alisisitiza kuwa yeye pamoja na viongozi wenzake watafanya kazi kwa karibu na mwajiri kwa lengo la kutatua masuala mbalimbali ya watumishi kwa wakati ili kuepusha mogogoro isiyokuwa ya lazima kati ya mwajiri na wafanyakazi.

Uchaguzi huo ulihudhuriwa na Afisa Tawala Mkuu kutoka Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Tume ya Utumishi wa Walimu, Omar Ilyas ambaye alimwakilisha Mwajiri.



*Picha ya pamoja ya viongozi wapya wa TUGHE Tawi la TSC mara baada ya kumaliza uchaguzi wa viongozi wa tawi hilo. Pichani, wa kwanza kutoka kulia kwa waliokaa ni mwakilishi wa mwajiri katika uchaguzi huo, Omar Ilyas akifuatiwa na Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma ambaye alikuwa msimamizi wa uchaguzi huo, Anter Tarimo, Mwenyekiti mpya wa tawi hilo, Francis Gwankisa (wa tatu kutoka kulia) akifuatiwa na Katibu wa tawi hilo, Enid Geofrey.*

# MICHEZO SHULENI NI SEHEMU MUHIMU KATIKA MAENDELEO YA WATOTO, JAMII NA UCHUMI WA NCHI – SERIKALI

- *Jitihada za uimarishaji miundombinu na ufundishaji wa somo la elimu kwa michezo na michezo katika ngazi zote za elimu zafanyika*
- *TSC yawakaribisha wadau mbalimbali wa Serikali kusaidia kutoa huduma kwa walimu katika eneo la utoaji elimu.*

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**





Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli amesema kuwa michezo ni sehemu muhimu katika maendeleo ya jamii na uchumi hivyo Serikali hivi sasa inafanya jitihada za kuimarisha ufundishaji wa somo la Elimu kwa Michezo na Michezo katika ngazi zote za elimu, kujenga shule maalumu za michezo, kujenga miundombinu ya michezo na kununua na kusambaza vifaa mbalimbali vya michezo.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli akifunga kikao kazi cha siku tatu cha asasi zinazotoa huduma katika eneo la elimu kilichofanyika jijini Dodoma.

"Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa wadau wanaotoa huduma katika eneo hili la elimu michezo na michezo, na kutokana na umuhimu wake, tunatoa wito wa wadau kuona uwezekano wa kuunga mkono jitihada za Serikali hasa katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo katika shule zetu, upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada kuhusu Elimu kwa Michezo, vifaa vya michezo



kwa wanafunzi wa kawaida na wenye mahitaji maalumu, na mafunzo kwa walimu wa michezo." Alisema Mweli.

Naibu Katibu Mkuu huyo anayeshughulikia eneo la Usimamizi wa Elimu kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inatarajia kuwa wadau watatumia vyema fursa ya mashauriano inayotolewa na Serikali katika hatua mbalimbali za maandalizi na utekelezaji wa miradi ili kuendana na kauli mbiu ya kikao kazi hicho iliyosema; "tupange na kutekeleza kwa pamoja miradi yenye tija kwa maendeleo ya Elimumsingi."

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama, akihitimisha wasilisho la mada kuhusiana na Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu aliwakaribisha wadau mbalimbali wakiwemo asasi zisizokuwa za Serikali kusaidia kutoa huduma kwa walimu katika eneo la utoaji elimu juu ya Maadili, Miiko na Maendeleo ya Walimu pamoja na Tafiti za masuala ya utumishi wa walimu nchini.

Akifunga kikao kazi hicho Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Gerald Mweli, alizishukuru na kuzipongeza asasi zote zilizoshiriki pamoja na Serikali kwa kuitikia wito na kudhamini Kikao Kazi hicho ikiwa ni pamoja na; Children in Crossfire (CiC), Project Concern International (PCI), Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Light for the World, Aga Khan Foundation (AKF), Data Vision Tanzania, World Education Inc., Social Action Trust Fund (SATF), Research Triangle Institute (RTI), na Young Scientists kwani huo ni mwanzo wa ushirikiano kwa maendeleo ya watoto na Taifa kwa ujumla.





# SUMA JKT YAWASILISHA MCHORO WA JENGO LA OFISI ZA TSC



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (mwenye miwani) akiongoza kikao cha kupitia mapendekezo ya mchoro wa jengo la TSC linalotarajiwa kujengwa katika eneo la Chinyoyo jijini Dodoma. Kikao hicho kilifanyika Agosti 25, 2021 katika ukumbi wa TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Mhandisi kutoka Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), Monica Mollel akiwasilisha mapendekezo ya mchoro wa jengo la ofisi za TSC Makao Makuu kwenye menejimenti ya TSC.*

**Na Mwandishi Wetu.**

Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) limewasilisha kwenye Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mapendekezo ya mchoro wa jengo la ofisi ya Tume hiyo ikiwa ni sehemu ya kukamilisha taratibu za kuanza kwa ujenzi wa ofisi hiyo katika eneo la Chinyoyo, jijini Dodoma.

Akiongoza kikao hicho kilichofanyika Agosti 25, 2021 katika ofisi za TSC Makao Makuu, Katibu wa Tume hiyo, Paulina Nkwama alieleza kuwa kikao hicho kilikuwa ni muhimu kwa upande wa mkandarasi (SUMA JKT) na Mteja ambaye ni TSC katika kujenga uelewa wa pamoja wa kile kinachotakiwa kufanyika.



*Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) pamoja na wataalamu wa ujenzi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI wakisikiliza wasilisho la mchoro wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu kutoka kwa Mhandisi wa SUMA JKT, Monica Mollel.*

# SUMA JKT YAWASILISHA MCHORO WA JENGO LA OFISI ZA TSC



*Mwonekano wa sehemu ya mbele wa jengo la ofisi ya TSC Makao Makuu kama ilivyowasilishwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).*

"Kikao hiki ni muhimu kwetu sote kwa kuwa mteja anakuwa na matarajio ya jinsi anavyotaka mradi wake ufanyike na mkandarasi naye anatakiwa atueleze uhalisia wa kile kitakachofanyika. Hivyo kabla hatujaanza kutekeleza mradi ni muhimu kila upande kupata picha halisi ya kile kinachokwenda kufanyika," alisema Nkwama.


Katika walisisho lililofanywa na Mhandisi kutoka SUMA JKT, Monica Mollel alieleza kuwa mchoro wa jengo hilo ambalo linatarajiwa kuwa na ghorofa tatu kwa kiasi kikubwa umezingatia mahitaji muhimu kama yalivyowasilishwa na TSC.

Baada ya kupitia kwa kina mchoro wa jengo hilo, Menejimenti ya TSC ilipata fursa ya kufanya maboresho kadhaa ili kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya Ofisi yanazingatiwa wakati wa ujenzi.

Mradi wa ujenzi wa jengo la Tume unatarajiwa kuanza hivi karibuni ambapo kukamilika kwake kutaifanya TSC kuwa na ofisi zake yenyewe tofauti na sasa ambapo imepanga katika moja ya majengo yaliyopo Mtaa wa Mtendeni jijini Dodoma.



*Mwonekano wa sehemu ya nyuma wa jengo la ofisi ya TSC Makao Makuu kama ilivyowasilishwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).*



*Mwonekano wa sehemu ya juu wa jengo la ofisi ya TSC Makao Makuu kama ilivyowasilishwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).*



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***